**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA**

# TANGAZO

**05/07/2024**

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa inatarajia kupangisha vibanda vya biashara 10 vinavyozunguka ukuta wa soko la Nafaka Kibaigwa, Yeyote mwenye nia ya kuomba anakaribishwa kutuma maombi yake kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, S.L.P 57, Kongwa.

**Sifa za Mwombaji**

1. Awe raia wa Tanzania
2. Awe mfanyabiashara au anayetarajia kufanya biashara.
3. Aina ya biashara anayotaka kufanya.
4. Namba ya Mlipa kodi (TIN)
5. Awe na kitambulisho cha **NIDA** au Namba ya NIDA.
6. Nakala ya Vyeti vya usajili wa biashara/Katiba ya kampuni kwa Makampuni.
7. Awe na leseni ya biashara au awe tayari kukata leseni mara tu baada ya kuingia katika kibanda cha biashara.
8. Awe tayari kusaini Mkataba wa Mwaka mmoja wa upangaji na Halmashauri.
9. Awe tayari kulipa Kodi ya pango ya Shilingi 150,000 kwa Mwezi.
10. Asiwe Mtumishi wa Umma au Kiongozi wa Siasa.
11. Barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa kata yake.

Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 08/07/2024 saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9.30 alasiri na Mwisho wa kupokea Maombi ni tarehe 17/07/2024. Saa 9.30 Alasiri.

..........................................

**Dr OMARY A. NKULLO**
**MKRUGENZI MTENDAJI**
**WILAYA YA KONGWA**

***MAOMBI YOTE YAAMBATANISHWE NA NAKALA INAYOTHIBITISHA SIFA ZA MWOMBAJI.***

***Tangazo hili linapatikana pia katika tovuti ya Halmashauri www.kongwadc.go.tz.***

CamScanner